**African Entrepreneurs – Successful and Responsible**

**Episode 08**

**Title: The Organic King – Jean Pierre Imelé from Cameroon**

**Author: Henri Fotso**

**Editor: Katrin Ogunsade, Adrian Kriesch**

**Translator: Salamata Saenger**

**Proofreading: Natalie Glanville-Wallis**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters (O-Töne, Clips) / Narrators**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| Intro/Outro | x | | Unimportant | |
| Narrator | | x | Unimportant | |
| Jean Pierre Imelé (clip) | | x | 54 | French |

**Pronunciation as it would be in German:**

Jean Pierre Imelé (Jong Pjär Imeleeh)

Buea (pronounced as written)

**<u>INTRODUCTION</u>:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya “Learning By Ear”, Noa Bongo, Jenga Maisha yako tukiwaangazia Wajasiriamali waliofaulu katika shughuli zao barani Afrika na mchango wanaotoa kusaidia maendeleo miongoni mwa jamii wanamoishi.Katika makala ya leo tunamuangazia Jean Pierre Imele, mkulima amepindukiwa kupata umaarufu sana kutokana na shughuli zake za kilimo cha kutumia Mbolea asilia nchini Cameroon.

1. **SFX: Ceaseless crackling of computer keyboard – Street noise from outside**

2. **Narrator:**

Tunakutana na mkulima huyu anayeonekana mwenye shughuli nyingi ofisini mwaka iliyoko Mji mkuu wa Duala. Japo tumefika ofisini mwake anajitia hamnazo kuwepo kwetu ofisni humo. Ni dhahiri kwamba kelele za magari barabarani zinazopitia dirisha la ofisini na hata mlangoni pia hazionekani kumtatiza hata kidogo. Akiendelea na kazi kwenye Komputa yake bila ya hata kutaka kuwajulia hali wageni waliofika ofisini, tunaamua kumkatiza kwa muda.

3. **Narrator :** Habari ya asubuhi!

4. **Jean Pierre Imelé :** Ni nzuri!

5. **Narrator :** Unaitwa nani?

6. **Jean Pierre Imelé :** Jina langu ni Jean Pierre Imele

7. **Narrator :** Una umri gani?

8. **Jean Pierre Imelé :** Nitafikisha miaka 54 tarehe 21 mwezi Agosti mwaka huu.

9. **Narrator :** Unafanya kazi gani?

10. **Jean Pierre Imelé :** Mimi ni mkulima. Kilimo cha kutumia mbolea asilia nchini Cameroon

11. **Narrator:**

Tunashangazwa na jibu hili kutoka kwa Mtu anayedai kuwa ni mkulima ilhali anafanya kazi ofisni. Kawaida utawapata wakulima wengi barani Africa wakiwa shambani wakati wingi. Na kwa kutazamana jinsi alivyoizoea Komputa na huku vitabu na faili vikijaa kwenye makabati ofisini humo,bila shaka hutaamini kuwa ni mkulima wa kawaida barani Afrika.

Kwa kuitikia mwito kuhusu mabadiliko kote ulimwenguni, Jean Pierre Imele ameanzisha mpango wa kilimo cha ukuzaji mimea kwa njia ya kisayansi kinachozingatia usafi wa Mazingira Biotropical. Tangu mwaka wa 1988, mazao yanayotoka shambani mwake yamepata soko kubwa cnhini Cameroon na hata katika soko la Kimataifa.

12. **Jean Pierre Imelé**

“Biadhaa za kampuni yetu zimepata umaarufu sana katika soko la humu na hata mataifa ya kigeni. Tuna jumla ya wafanyi kazi 200 wanaofanya kazi katika shamba la ukubwa wa ekari 400. Kawaida hupanda mazao katika ardhi ya ekari 200 na kuongeza ekari hizo kila mwaka. Tunapanda mazao kama vile Maembe, na kama unavyofahamu, maembe ya rangi ya kijani kibichi yanayokuzwa nchini Cameroon ni matamu, ni matamu sana. Pia tunakuza mananasi, ndizi na papai mbali na maboga na matunda katika shamba letu.”

13. **Narrator:**

Kulingana na Jean Pierre Imele, kilimo hiki cha kutumia mbolea asilia kina faida sana na ni rahisi kukistawisha. Ingawa gharama zake ni kubwa

14. **O-Ton: Jean Pierre Imelé (fr.)**

"Bado tunakumbwa na changamoto nyingi sana. Tunataka kuimarisha mbinu za uzalishaji ili kutambua kwa urahisi matatizo yanayoambatana na shughuli za uzalishaji mazao hayo. Kama kawaida mbolea huleta wadudu wa kila aina mfano nzi wanaopenda sana maembe".

15. **Narrator:**

Lakini kilimo cha kutumia Mbolea asilia hakihitaji kunyunyuzia dawa za kukabiliana na wadudu waharibifu kama ilivyo miongoni mwa wakulima wengi. Kilimo hiki cha Mbolea asilia ni aina ya kilimo kisichohitaji matumizi ya kemikali. Katika bara Ulaya kilimo cha mashamba makubwa makubwa hutumia sana mbolea za kemikali na kila mara kunyunyuzia dawa za kuuawa wadudu. Lakini watu wengi wanapendelea sana vyakula ambavyo vinakuzwa kwa njia asilia. Na vyakula vya asilia ni vitamu zaidi. Hii ndio sababu wakulima wengi hupenda kutumia pesa nyingi kwa mbolea asilia. Pia hii ndio sababu matunda yanayokuzwa barani Africa kwa kutumia mbinu hizi za kilimo kawaida yanasoko kubwa sana barani Ulaya kuliko hapa kwetu Afrika. Jean Pierre Imele anapata pato kubwa sana kutokana na mauzo yake katika soko la kigeni hali inayomwezesha kubuni nafasi zaidi za kazi kwa vijana wengi Barani Africa. Alipokuwa akisoma ng'ambo, Jean Pierre Imele alikuwa na hamu sana ya kuwa mkulima ili kuchangia katika maendeleo ya nchi yake. Hata hivyo lakini imekuwa safari ndefu.

16. **Jean Pierre Imelé**

“Nilikuwa na umri wa miaka 18 wakati niliposafiri kwenda nchini Ufaransa. Niliwasili mjini Lyon na kama ilivyokawaida ya wageni wengi wanaowasili nchini humo, nikatuma maombi ya kujiunga na chuo kusomea masuala ya usimamizi wa biashara, pamoja na masuala ya uchumi, usimamizi na sheria. Niliondoka chuoni humo baada ya muda wa miaka miwili. Kisha nikaenda kujiunga na chuo maalum kwa masomo zaidi kuhusu utayarishaji mazao,utabiri wa hali ya hewa na masuala ya biashara. Nilitaka kujifunza mambo yote ili niweze kuwa mtaalam katika nyanja zote zinazohusiana na kilimo kama ninachotekeleza hapa.”

17. **Narrator:**

Baada ya kufanya kazi kwa muda wa miaka 23, Jean Pierre Imele anasema bado kuna changamoto mbili zinazomkumba. Ya kwanza ni jinsi ya kuimarisha mbinu za uzalishaji ili kutosheleza mahitaji ya wateja wake.

18. **Jean Pierre Imelé**

“Kwa upande mwengine nataka kuimrisha ubora wa bidhaa kutoka Afrika. Tuna rasilimali nyingi sana hapa Barani Africa. Tunaweza kusema Afrika ni jungu la rasilimali na linauweza mkubwa wa maendeleo, mfano katika sekta ya kilimo ambayo bado iko nyuma sana. Changamoto nyingine ni kutoa ufahamu kwa vijana kuhusu umuhimu wa kilimo, kwamba wanaweza kujiendeleza maishani kupitia kilimo. Hebu nitazame, nina dereva anayenipeleka, licha ya kwamba ni mkulima tu.”

19. **Narrator:**

Lakini Mtu hawez kupata ufanisi bila ya kujitolea. Jean Pierre Imele amejitolea kufanya kazi kwa bidii sana.

20. **Jean Pierre Imelé**

“Hakuna jambo rahisi. Tangu nianzishe biashara hii,mimi hufanya kazi kwa masaa 15 kwa siku. Na ninafurahia sana kazi yangu. Pia ninafanya utafiti kustawisha kilimo na kusimamia vyema mbinu za ukuzaji na mavunaji”

21. **Narrator:**

Kwa Jean Pierre, kumiliki gari kubwa au vitu vya thamanin si chochote kwake. Utajiri wake ni fahari ya kuweza kumiliki shamba kubwa la maembe na mazao mengineyo. Na ndio maana anamatarajio makubwa kutoka kwa wafanyi kazi wake.

22. **.Jean Pierre Imelé**

“Mimi huwaamrisha wafanyakazi wangu. Sijui kama huo ni upungufu au ndivyo inavyotakikana, lakini napenda kuona tukisonga mbele pamoja. Yaani wajitolee kufanya kazi kama ninavyojitolea mimi. Mimi ni binadamu kama wengine na hivyo naelewa kwamba binadamu wote si sawa. Pia mimi nina mapungufu kama binadamu wengine(laugh)”.

**23. SFX: crackling of computer keyboard**

24. **Narrator:**

Kufanya mambo mengi kwa wakati mmoja si tatizo kwake, na hapa anaendelea na kazi katika komputa kutafuta soko la mazao yake.

25. **Jean Pierre Imelé**

Mimi huwashauri vijana kuzingatia zaidi shughuli za kilimo na kushirikiana kuanzisha miradi kama hii. Usitake kufanya kila kitu peke yako. Ni vyema kuwa na kundi la washirika wa kutegemewa, kwani mara nyingine unaweza kukumbwa na changamoto mfano tatizo la mashine, na mnapo kuwa washirika na wengine ni rahisi kubadilishana mawazo na kuendeleza shughuli zenu za kilimo ili kushindana kikamilifu na mataifa mengine, mfano Vietnam, Brazil ambazo zinafahamika sana kwa shughuli za kilimo.

26. **Narrator:**

Kwa Jean Pierre msingi wa ufanisi hutegemeza ari ya Mtu kufanikisha mradi wowote ule. Pesa sio hoja aliweza kuansiha mradi wake kwa mtaji mdogo sana wa kima cha Euro 1500 tu. Na sasa mradi huo unamletea pato la jumla ya Euro 800,000 mbali na kubuni nafasi za kazi kwa watu wengi sana . Kulingana na Mkulima huyu, sekta ya Kilimo inauweza kubuni ajira kwa viana wengi barani Afrika.

27. **Jean Pierre Imelé**

Tuna bahati hapa barani Afrika kwani tuna ardhi kubwa amabyo haitumiki kikamilifu, mazingira bora ya uzalishaji, idadi ndogo ya watu ikilinganishwa na mabara mengine na mito isiyokauka kila mahali.Iwapo serikali za Afrika zingeweza kuratibu mageuzi katika sekta ya kilimo sera nzuri kuhusu matumizi ya ardhi Watu wengi maskini wangeweza kumiliki ardhi na kustawisha mashamba yao. Hii ndio njia pekee ya kupambana na baa la njaa.

**28. SFX: Sound effects of cars and passer-by on the street**

29. **Narrator:**

Ni saa tisa alasiri na tayari wafanyi kazi wengi mjini Duala wameanza kutoka ofisni ili kutoroka msongamano wa magari barabarani. Lakini Jean Pierre bado hana haraka kufunga ofisi hadi atakapokamilisha kazi yake. Je atakubali kutenge muda mchache kuandamana nasi kwa chakula cha jioni. Kwanza ana guna na kisha kukataa ombi letu.

30. **Jean Pierre Imelé**

« Unajua nimewasili jana usiku kutoka Italy kuhudhia mkutano kuhusu mpango wa utafiti wa kilimo barani Africa.Nimekuwa nje kwa zaidi ya muda wa siku 10, kwani pia nilikuwa nahudhuria maonyesho ya biashara nchini Japan kabla ya kuelekea Italy. Nafikiri nitafanya kazi hadi mwendo wa saa nne hivi za usiku.Nataka kumaliza kazi yote, kwani kuna utulivu na hakuna shughuli nyingi baada ya wafanyi kazi wengi kuondoka kwenda nyumbani. Lakini siku nyingine za kawaida mimi hufanya kazi masaa ya kawaida na kwenda nyumbani mapema. Wakati wa likizo huependa kwenda sehemu zenye milima au baharini kupumzika. Na ndio maana nikaamua kujenga makao yangu katika sehemu ya Buea iliyoko chini ya mlima Cameroon. Na mara nyingine hufanya mazoezi ya kukwea mlima pamoja na rafiki zangu.""

31. **Narrator:**

Hivyo tukakubaliana kukutana naye nyumbani kwake Buea katika muda wa siku mbili sijazo. Familia yake ilitupokea kwa furaha nyumbani ambayo ni mwendo wa dakika chache kwa gari dogo kutoka ufuo wa bahari. Na kisha tukakaribishwa sebuleni na kurejelea tena mazungumzo yetu kuhusu kilimo kinachotumia mbolea asilia.

**32. SFX: kitchen sounds and children in the background**

Huku Mkewe akijishughulisha na mapishi jikoni, watoto walikuwa wakicheza nje ya nyumba yao. Jean Pierre anatueleza kuhusu mipango yake ya baadaye ambapo anapanga kusafiri kwenda Ujerumani na kuahidi kututembeza shambani mwake pindi atakaporudi. Kwa sasa tunaonja utamu wa vyakula vilivyokuzwa kwa mbolea asilia katika shambani lake ambavyo tumeandaliwa chakula cha jioni.

**Outro:**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa makala yetu leo ya Learning by Ear ambapo tumemuangazia Mkulima Jean Pierre Imele anayetumia mbolea asilia kukuza vyakula nchini Cameroon. Mwandishi wetu ni Henri Fotso, Tunakushukuru wewe msikilizaji wa kwa kutega sikio na iwapo ungependa kukisikiliza tena kipindi hiki au kutuma maoni tembelea mtandao wetu wa www.dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine tutakapokutana tena kwa makala mengine Kwaheri kwa sasa.